



Dkt. Devon Q. Horton, *Msimamizi*

SWAHILI

Bw. Dijon DaCosta, Sr., *Mwenyekiti wa Bodi*
Bi. Deirdre P. Pierce, *Makamu Mwenyekiti*
Bi. Anna Hill
Bi. Whitney McGinniss
Bi. Allyson Gevertz
Bi. Vickie B. Turner
Dkt. Joyce Morley

INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA

Tarehe 12 Machi 2024

Wasiliana na:

Donald Porter, *Ed.D.*
Carla Parker

678-481-4110
404-734-1717

**Ukaguzi wa Hivi Majuzi wa Shirika la Cognia Wadhihirisha Utawala
Bora wa Bodi na Kujitolea kwa Uboreshaji Endelevu**

(STONE MOUNTAIN, GA) – Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) ina furaha kutangaza matokeo bora ya Ripoti ya hivi majuzi ya Ukaguzi wa Ufuatiliaji wa Shirika la Cognia. Ripoti hiyo inaonyesha kuwa uongozi wa Wilaya unatekeleza majukumu na wajibu wake kwa kuzingatia viwango vya utawala.

Tathmini hiyo iliyofanywa kuanzia tarehe 1 hadi 3 Novemba 2023, ilinua kutathmini maendeleo ya DCSD katika kushughulikia Kiwango cha 1.5 cha Utendaji cha Cognia kutoka itifaki ya awali ya uidhinishaji na maelekezo hayo yalioana na kiwango hicho kutoka kwa ukaguzi wa ufuatiliaji uliofanywa tarehe 8 hadi 11 Novemba 2022. Maboresho hayo yalisherehekewa na uongozi wa Wilaya.

“Ukaguzi wa COGNIA wa maendeleo na utawala wa Bodi ya Shule ya Kaunti ya DeKalb ni dhihirisho la kujitolea kwao thabiti katika ufaulu wa wanafunzi. Kwa kujitolea kwa uboreshaji endelevu, wameleta hali ya kimageuzi ya kielimu ambayo inawawezesha wanafunzi kufanikiwa kimasomo, kijamii na kihisia,” alisema Msimamizi wa DCSD Dkt. Devon Q. Horton. “Uongozi wao wenye maono na mbinu shirikishi umeweka kiwango kipya cha ubora wa kielimu, na kuwafanya kuwa kielelezo cha kweli kwa bodi za shule nchini kote.”

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufuatiliaji wa Cognia ilionyesha alama “inayoboreka” kuhusiana na kiwango cha utawala wa Bodi. Hasa zaidi, ilisema, “Bodi inalenga zaidi kushirikiana pamoja kwa manufaa ya wilaya na, hasa, kwa ajili ya mafanikio ya wanafunzi.” Ripoti hiyo ilisema, “Wajumbe wa Bodi walikuwa na shauku juu ya jukumu lao, na wengi walitekeleza jukumu kubwa katika kufuata sera na taratibu zilizowekwa.”

“Bodi ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb imefurahishwa na matokeo ya ukaguzi huu wa hivi majuzi kutoka shirika la Cognia, lakini tunatambua kuwa kuna kazi zaidi inayohitaji kufanywa,” alisema Mwenyekiti wa Bodi Bw. Dijon DaCosta, Sr. “Inadhihirisha zaidi juhudi nyingi za Bodi hili katika kuimarisha na kuendeleza wilaya ya kipekee ya shule za umma. Bodi ya Elimu ya Kaunti ya DeKalb inaendelea kujitolea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuboresha utawala wa bodi na kuimarisha na kudumisha juhudi za sasa za kuboresha mustakabali wa wasomi wetu.”

-ZAIDI-

Ripoti hiyo ilitaja mkutano wa Bodi mnamo Februari 2023, ambapo wajumbe wa Bodi walikagua ripoti ya Novemba 2022 na kushughulikia matokeo na sehemu za uboreshaji katika ripoti hiyo.

“Mbali na mkutano wa Februari 2023, wajumbe wa bodi walikagua na kujadili matokeo ya Ripoti ya Ukaguzi wa Ufuatiliaji ya Novemba 2022 wakati wa kipindi cha biashara cha kawaida kilichoratibiwa cha mkutano wa bodi mnamo tarehe 19 Aprili 2023,” ripoti hiyo ilisema. “Maoni ya wajumbe yalikubaliana kwa kiasi kikubwa na matokeo na kupendekeza uwajibikaji zaidi kwa upande wao ili kuhakikisha uendeshaji wenye ufanisi kama bodi ‘kwa ujumla’.”

Ripoti ya Ukaguzi wa Ufuatiliaji wa Cognia ilihimiza DCSD itekeleze “hatua zifuatazo”:

- Ikague na ishiriki matokeo na wadau.
- Ihakikishe Bodi inatekeleza kikamilifu mbinu bora za utawala wa bodi kutoka kwa vipindi vya mafunzo ya kitaaluma.
- lendelee kurekebisha Mwongozo wa Wajumbe wa Bodi.
- Irekebishe na isasishe sera na taratibu mara kwa mara ili kuhakikisha zote ni za kisasa na zinafaa.
- landae Ukaguzi wake wa Ushirikishaji wa Uidhinishaji kabla ya tarehe 30 Juni 2027, kwa kuwa wilaya imetimiza matarajio ya Kiwango cha 1.5 cha Utendaji cha Cognia.

Cognia imeidhinisha kikamilifu DCSD hadi tarehe 30 Juni 2027. Cognia™, ni shirika lisilo la faida, lisilo la kiserikali linaloidhinisha shule za msingi na sekondari, na linahudumia zaidi ya taasisi 36,000 zenye wanafunzi milioni 25 na walimu milioni moja katika takriban nchi 80.

Ripoti kamili ya Ukaguzi wa Ufuatiliaji wa Cognia kwa DCSD inapatikana kwenye tovuti ya Wilaya [HAPA](#).

XXX